Tofauti na nyaraka nyingi za mtume Paulo, ambazo aliziandika kwa Makanisa, waraka huu aliuelekeza kwa Timotheo ambaye alisimama sio tu kama msaidizi wake wa kihuduma bali pia kama mwanae Katika vifungo vya injili. Ni waraka wa kichungaji zaidi ya wa kimafundisho,

Katika waraka huu Paulo anamwagiza Timotheo namna ambavyo kanisa linapaswa likae katika utaratibu, Mungu alioukusudia.(1Timotheo 3:15)

Maudhui makuu ya Paulo kwa Timotheo yalikuwa ni haya;

1. Kujilinda na waalimu wa uongo.
2. Namna ya ‘jinsia na marika’ mbalimbali yanavyopaswa yaenende/ kuhudumu ndani ya nyumba ya Mungu.
3. Vigezo vya viongozi thabiti wa kuliongoza Kanisa.
4. Agizo kwa Timotheo kuwa kamili katika utumishi wake.

Haya ni maelezo mafupi Kwa kila kipengele.

1) Kujilinda na waalimu wa Uongo.

Paulo anamhiza Timotheo lengo kubwa la kumtaka abaki Efeso ni ili awazuie watu wasifundishe elimu nyingine.

1 Timotheo 1:3

> *[3]Kama vile nilivyokusihi ukae Efeso, nilipokuwa nikisafiri kwenda Makedonia, ili uwakataze wengine wasifundishe elimu nyingine;*

Elimu hiyo potofu aliyoina iliegemea kuwazuia watu wasile aina ya vyakula, Wasioe, pamoja na kuhubiriwa Hadithi za kizee, na nasaba (1:4, 4:7)

Kwa urefu wa mafundisho Hayo bofya hapa >>> HADITHI ZA KIZEE.

1 Timotheo 4:1-3

> *[1]Basi Roho anena waziwazi ya kwamba nyakati za mwisho wengine watajitenga na imani, wakisikiliza roho zidanganyazo, na mafundisho ya mashetani;*
>
> *[2]kwa unafiki wa watu wasemao uongo, wakichomwa moto*

> *dhamiri zao wenyewe;*
>
> *[3]wakiwazuia watu wasioe, na kuwaamuru wajiepushe na vyakula, ambavyo Mungu aliviumba vipokewe kwa shukrani na walio na imani wenye kuijua hiyo kweli.*

2) Namna ‘jinsia na marika’ mbalimbali yanavyopaswa yaenende ndani ya Kanisa la Mungu.

*Kwa wanaume:* Paulo anatoa agizo la kwamba wao wanajukumu la kusalisha kila mahali, lakini bila hasira wala majadiliano, yaani wawe safi kiibada (2:8)

*Kwa Wanawake:* Paulo anatoa agizo kuwa hawana ruhusa ya kufundisha katika kanisa (2:12), halikadhalika wanawajibu wa kuvaa mavazi ya kujisitiri, mapambo yao yawe yale ya rohoni na sio ya mwilini (2:9-10).

Anaendelea kusema Wanawake ambao ni wajane waandikwe katika kanisa ili Wahudumiwe kimahitaji, lakini wale ambao si wajane kwelikweli hawapaswi kuandikwa (5:4-16)

*Wazee, na vijana* wafanyapo makosa wasikemewe, Bali Waonywe

kwa upole Kulingana na marika yao(5:1), lakini pale wafanyapo dhambi. kwa kukusudia au kuzoelea wakemewe mbele ya wote. (5:20),

*Watumwa wote* wanawajibu wa kuwaheshimu mabwana zao, si tu kwa wale wasiamini bali pia kwa wale waaminio wawaheshimu wote. (6:1)

Kanisa lina wajibu wa kuwaombea watu wote, na watawala, ili liishi katika utulivu, na amani, katika utauwa wote.(2:1-4)

3) Kuchagua viongozi thabiti wa kulichunga kanisa

Sehemu hii Paulo anamwagiza Timotheo juu ya vigezo vya maaskofu, na Mashemasi namna wanavyopaswa wawe, kwamba wawe watu wasio laumika, wameshuhudiwa mema na watu wa nje, waume wa wake mmoja mmoja, si watu wa kupenda fedha,si walevi, si waongofu wapya, wanapaswa wawe wakaribishaji,, wastahivu, wenye kiasi, waaminifu, wawasimamiao watoto wao vema, na wake zao, (3:1-13).

Lakini pia anawahimiza wazee wanaotawala vema wahesabiwe kuwa wamestahili heshima mara dufu (5:17).

4) Agizo la Paulo kwa Timotheo kuwa kamili katika utumishi wake.

Paulo anamwagiza Timotheo wajibu wake kama mwangalizi kuwa na upendo, Imani isiyo na unafki, na dhamiri njema, upole, saburi, na haki (1:5, 18-20, 6:11),

Anamwagiza afanye mambo yote bila upendeleo (1Timotheo 5:21).

Ajizoeshe kupata utauwa (4:8).

Awe kielelezo katika usemi na mwenendo (4:12)

Asiwaekee watu mikono kwa haraka,(5:22)

Akimbie tamaa ya fedha, na mashindano ya kidini (6:20).

Hitimisho.

Hivyo kwa ufupi, waraka huu ni wa kikanisa zaidi, na kwamba vigizo hivyo vikisimamiwa vema kanisa litakuwa imara, lenye heshima lisiloshitakiwa mabaya nje.

Ikiwa viongozi watachaguliwa hodari, na kila rika na jinsia likahudumu katika nafasi yake, yaani wanawake Kudumu katika upole, kujisitiri na kiasi na wanaume kuhudumu bila hasira wala majadiliano, huku waangalizi wakihakikisha mafundisho potofu hayapati nafasi. Ni ukweli kwamba kanisa hilo litakuwa imara sana.

Bwana akubariki

Shalom

Washirikishe na wengine habari hizi njema kwa kushea

Ikiwa utapenda kupata msaada wa kumpokea Yesu maishani mwako bure, Basi wasiliana nasi kwa namba uzionazo chini ya makala hii.

Pia kwa kupokea mafundisho ya kila siku kwa njia ya WHATSAPP, jiunge na channel yetu kwa kubofya link hii >>https://whatsapp.com/channel/0029VaBVhuA3WHTbKoz8jx10

Kwa mawasiliano: +255693036618 au +255789001312

Bwana akubariki.

Mada nyingine:

> *Nasaba ni nini kibiblia?(1Nyakati 9:1, Tito 3:9)*

> *Timotheo alikuwa wapi wakati anaandikiwa nyaraka zake na mtume Paulo?*

> *Je ni kweli Tumejengwa juu ya Mitume na Manabii? (Waefeso 2:20)*

> *JINSI ITAKAVYOKUWA KATIKA SIKU ILE*

Share on:
WhatsApp